

LAWYERS' ENVIRONMENTAL ACTION TEAM (LEAT)

*Research, Advocacy and Training on Environmental / Natural Resource Law and Policy and the
Promotion of Human Rights*
Website: <http://www.lead.or.tz>

Tel : +255 22 2780859
Fax : +255 22 2781098
Email : info@lead.or.tz
Website : [http //www.lead.or.tz](http://www.lead.or.tz)



Mazingira House, Plot No. 428
Mazingira Street, Mikocheni "B"
P. O. Box 12605
Dar es Salaam

Salamu za Siku ya Mazingira Duniani

Ndugu Wananchi

Mnamo tarehe 5 Mwezi Juni kila mwaka Dunia huadhimisha siku ya mazingira duniani. Ujumbe wa mwaka huu ni ***Uchafuzi wa Hewa: Hatuwezi kuacha kupumua lakini Twaweza kufanya kitu juu ya ubora wa hewa tuivutayo*** Maadhimisho ya kidunia yatafanyika nchini China.

China ni moja ya nchi zenye viwango vikubwa vya uchafuzi wa hali ya hewa duniani. Pamoja na mambo mengine, maadhimisho ya mwaka huu yanalenga kuzitaka serikali, hasa za nchi zenye viwanda, kuchukua hatua madhubuti ili kupunguza matumizi ya nishati ukaa ambazo si rafiki kwa mazingira. Uchafuzi wa hewa husababisha vifo vya mapema na gharama kubwa za kuwatibu na kuwauguza wagonjwa wa magonjwa yaletwayo na hewa chafu.

LEAT, kama mdau wa mazingira, itaadhimisha siku ya Mazingira Duniani kwa kutekeleza shughuli mbalimbali za uhifadhi na ulinzi wa mazingira.

Kwanza, LEAT kwa kushirikiana na Wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa itanza zoezi la uandaaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji vitano vinavyozunguka Ziwa Sundu. Ziwa Sundu ni muhimu kwa ustawi wa wananchi wanaolizunguka. Ziwa hilo ni chanzo muhimu cha maji kwa vijiji takribani sita.

Pili, LEAT kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bonde la Maji ya Ziwa Rukwa, imeandaa mafunzo ya wadau wa maji ili, pamoja na mambo mengine, kujenga uwezo wa wadau wa maji kuweza kupanga matumizi ya rasilimali za maji kwa weledi na kwa manufaa ya kizazi cha sasa bila kuathiri uwezo wa vizazi vijavyo kupata mahitaji yake. Utunzaji dumivu wa mabonde haya utachangia katika kutunza miti inayovuta na kuhifadhi hewa ukaa.

Sambamba na salamu hizi za Siku ya Mazingira Duniani, LEAT inapenda kuipongeza tena Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua yake ya kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki, maarufu kama rambo. Ila inataka juhudi kubwa zielekezwe kupambana na uchafuzi wa hewa unaofanywa na viwanda, magari, mioto, na vumbi. Aidha uchafuzi wote wa mazingira lazima upigwe vita.

Wito wetu kwa watanzania ni kutumia na kutunza mazingira yetu kwa njia iliyo dumivu na endelevu. Bila mazingira safi na salama maendeleo ni kujiangamiza wenyewe.

Imetolewa mjini Dar es Salaam leo tarehe 4 Juni 2019



Dk. Rugemeleza A.K. Nshala
Mkurugenzi Mtendaji